# MWONGOZO HUU WA KUSOMA BIBLIA NYUMBANI

Umetungwa na
Carroll Shaw

UTANGULIZI UMETUNGWA NA
Claylan Coursey

Mpango Rahisi Wa Kuongeza Kanisa
au Kuanzisha Kanisa Jipya

# MWONGOZO HUU WA KUSOMA BIBLIA NYUMBANI


Masomo Yametungwa

na

CARROLL SHAW

UTANGULIZI UMETUNGWA NA

Claylan Coursey

Kutafsiriwa Katika Kiswahili

na

Gabriel S. K. Mwavuo
Jackson Yeri
Nathaniel J. Baya



Masomo Yameruhusiwa Kutumika na
Dr. Carroll Shaw na
Southwestern Baptist Theological Seminary
Fort Worth, Texas

Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

## YALIYOMO


UTANGULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

MWONGOZO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 3

MASOMO

Somo la Kwanza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 5
Somo la Pili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 7
Somo la Tatu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 9
Somo la Nne . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 11
Somo la Tano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 13
Somo la Sita . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 15
Somo la Saba . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 17
Somo la Nane . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 19
Somo la Tisa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 21
Somo la Kumi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 23
Somo la Kumi na Moja . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 25
Somo la Kumi na Mbili . . . . . . . . . . . . . . . . . . 27
Somo la Kumi na Tatu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 29
Somo la Kumi na Nne . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 31
Somo la Kumi na Tano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 33
Somo la Kumi na Sita . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 35
Somo la Kumi na Saba . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 37

# UTANGULIZI

Kuna njia nne za kutumia mpango huu. Kwanza, unaweza kutumiwa kama kifaa cha uinjilisti kwa kuongeza washiriki katika kanisa lenyewe. Pili, unaweza kutumiwa kwa kuanzisha kanisa jipya. Tatu, unaweza kutumiwa pamoja na kitabu, Maisha Yako na Kanisa Lako, kufundisha waamini wapya kukusaidia kuanzisha tabia ya kusoma Biblia na maombi kila siku.

Nne, unaweza kutumiwa na yule Mkristo mpya kama chombo cha kushuhudia jamii yake na pia wale marafiki waliopotea. Wakati alipoamini, Mkristo huyu mpya huwa na hamu sana ya kuzungumza juu ya imani yake mpya aliyoipata karibuni na huwa anafahamu watu wengi walio wapotevu kushinda nyakati nyingine zote za baadaye. Jambo hili linaweza kumsaidia kuwaleta katika imani ya Yesu ijapokuwa yeye hana mafunzo ya kutosha katika kuhubiri (uingilisti).

Kwa kutumia mpango kuongeza kanisa, mshiriki au kundi la washiriki laweza kutumia taratibu hii katika namna hii. Wanaweza kutafuta mji au jamii iliyo haiendi kanisani walio watawakubalia nao kufika kila mara kusoma Biblia pamoja hapo nyumbani kwao. Hii inaweza kuwa kwa kila siku au baada ya siku mbili au tatu ama siku moja kwa juma zima mpaka mara kumi na saba. Kwa kufuata mpango huu wa kusoma Biblia nyumbani wanaweza kusaidia watu wa mji ule kutambua mpango wa Mungu katika maisha yao. Wataweza kutambua hali yao ya dhambi, na ya upotevu, kipawa (zawadi) cha Mungu kwao, na maisha mapya yanayopatikana katika Yesu Kristo. Kama wanavyoendelea kuamini na kumpokea Kristo Yesu, wanaweza kuongezwa kwa kanisa.

Kwa kutumia kuanzisha kanisa jipya, washiriki wa kanisa hilo wanaweza kwenda katika sehemu iliyo haina kanisa lililo la imani yao. Hapo wanaweza kutafuta mji au jamii iliyo itawaruhusu hao au kuwakaribisha kuanzisha masomo ya Biblia. Mji huu au jamii hii inaweza kuwakaribisha majirani wao kufika pale pia. Hapa

pia mpango huu unaweza kufuatwa kila siku, au kila siku **mbili**, au tatu ama mara moja kwa juma. Kuanzia katika siku ya tatu na ya nne katika kuwatembelea hawa, yule kiongozi anaweza kuwauliza kabla ya kuondoka pakiwa pana mtu ye yote anayependa kuombewa au kuomba ili ampokee Yesu Kristo katika maisha yake awe Bwana wa maisha yake.

Inapofika katika ile siku ya kumi na saba, wengi watakuwa wamekwisha kumpokea Yesu Kristo. Hawa wote waliomkubali Yesu Kristo watapenda kuwa kanisa jipya. Kanisa lile dhamini litaendelea kuwapa mwongozo na mafundisho kundi hili changa mpaka watakapokuwa wapevu wa kutosha kujiongoza wenyewe.

Itakuwa jambo zuri au jambo la busara pakiwa patakuwa na vitabu vya Agano Jipya vya kutosha kupewa kila mtu yule aliye anaweza kusoma atumie. Itasaidia ikiwa kanisa linaweza kupanga kumpa kitabu cha Agano Jipya kwa kila msomaji anayehudhuria kikao (darasa) hilo kwa uaminifu.

Taratibu ya kila siku inafuatwa hivi.

1. Soma wazi wazi Maandiko Matakatifu ya siku hiyo.
2. Soma kifungu kikuu cha Maandiko.
3. Soma maelezo kuhusu kifungu kikuu cha Maandiko.
4. Soma kila swali na lipe nafasi hilo kundi lizungumze juu ya swali hilo.
5. Soma maelezo ya mwisho.
6. Soma vifungu vyote vya siku hiyo tena.
7. Omba.

Kwa kufaulu katika kutumia mpango huu wa kusomea Biblia nyumbani kuwavuta watu kwa Yesu Kristo, mtu anahitaji awe na uwezo wa kusoma Biblia wazi tu ili wengine waweze kumfahamu. Yule kiongozi lazima achukue mazoezi ya kusoma Maandiko kwa sauti kwa mara nyingi kabla ya kwenda kwa darasa au kikao kile. Ye yote mshiriki wa kanisa aliye anaweza kusoma anaweza kutumia taratibu hii na kuwa mtu wa kuleta wengine kwa Yesu. Biblia itajishuhudia yenyewe wakati inaposomwa.

MWONGOZO HUU WA KUSOMA BIBLIA NYUMBANI

| MKUTANO | ANDIKO | SOMO |
|---|---|---|
| 1 | Warumi 3:21-31<br>Kifungu Kikuu - 23 | WOTE NI WENYE DHAMBI |
| 2 | Warumi 6:1-23<br>Kifungu Kikuu - 23 | ADHABU |
| 3 | Yohana 3:1-21<br>Kifungu Kikuu - 16 | UPENDO WA MUNGU |
| 4 | Warumi 10:1-11<br>Vifungu Vikuu - 9-10 | KUKIRI |
| 5 | 1 Yohana 5:1-13<br>Vifungu Vikuu - 11-12 | HAKIKISHO |
| 6 | 1 Wakorintho 10:1-14<br>Kifungu Kikuu - 13 | USHINDI |
| 7 | Warumi 8:24-39<br>Kifungu Kikuu - 30 | WOKOVU NI WA MUNGU |
| 8 | Wagalatia 3:1-29<br>Kifungu Kikuu - 13 | NEEMA YA MUNGU |
| 9 | Yohana 10:7-30<br>Kifungu Kikuu - 30 | KRISTO NA MUNGU |
| 10 | Luka 15:11-32<br>Vifungu Vikuu -21,22,24 | KUSAMEHEWA |
| 11 | 1 Wakorintho 3:1-23<br>Vifungu Vikuu - 9-11 | UKRISTO |
| 12 | Waefeso 4:17-6:9<br>Vifungu Vikuu - 4:22-24 | ASILI MPYA |
| 13 | Yohana 14:1-21<br>Kifungu Kikuu - 6 | NJIA |
| 14 | Matendo 2:14-41<br>Kifungu Kikuu - 38 | TOBA |
| 15 | Matendo 8:26-39<br>Kifungu Kikuu - 37 | KUJIKABIDHI |
| 16 | Matendo 16:14-36<br>Kifungu Kikuu - 31 | AMINI |
| 17 | 1 Yohana 1:1-10<br>Kifungu Kikuu - 9 | UNYENYEKEVU |

# WOTE NI WENYE DHAMBI

MAANDIKO: Warumi 3:21-31

KIFUNGU KIKUU: Warumi 3:23. "Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."

## WOTE:

Wote ni neno linalotaja kila mtu. Biblia inazungumzia juu ya Yesu, Mwana wa Mungu, kuwa ni yeye tu peke yake hakuwa na dhambi. Ingawaje tunaweza kujisifu kuwa hatuna dhambi, lakini hata hivyo mioyo yetu bado inatushitaki.

Mwanadamu alichagua dhambi. Mungu alipomweka mtu mume na mtu mke duniani, walikuwa ni wakamilifu. Walijaribiwa na Shetani. Walishindwa na majaribu haya. Kama watoto wadogo, twajua tufanyapo makosa.

Dhambi hututenganisha na Mungu. Hii ina maana ya kila mtu azaliwaye. Hachagui rangi ya mtu, elimu ama utajiri.

## WAMEFANYA DHAMBI:

Hii ni kuchagua njia yetu binafsi. Tunafanya mambo yasiyopendeza kwa Mungu. Dhambi yetu kubwa ni kumkataa Yesu kama Mwokozi wetu. Twafanya uasi kwa Mungu. Twajaribu kuishi vile tutakavyo. Hii inatufanya tujisikie kuwa wenye hatia mioyoni mwetu.

## KUPUNGUKIWA:

Dhambi zetu hututenganisha na Mungu. Wakiwa na dhambi, Adamu na Hewa waliona haya kusimama mbele za Mungu. Mungu ni mtakatifu

hivyo dhambi haiwezi kusimama mbele zake. Tukiwa na dhambi zetu sisi si watu wale ambao Mungu alikusudia tuwe.

UTUKUFU WA MUNGU:

Mungu anataka tushirikiane naye. Anataka tuishi na kuonyesha njia yake ya maisha. Mungu hapendi (hukataa) dhambi. Mtoto afanyapo makosa hana furaha kuwaona wazazi wake. Mtoto hujisikia ana hatia moyoni.

Utukufu na wema wa Mungu hutushitaki mioyoni mwetu. Katika dhambi tunapungukiwa na vile Mungu atakavyo tuwe. Anatutaka sisi tuwe katika utukufu wake.

MASWALI:

1. Je! Neno "wote" lahusu watu wangapi?

2. Je! Twaweza kujua tufanyapo dhambi?

3. Twabainishaje kati ya haki na makosa?

4. Dhambi ni nini?

5. Je! Mungu hututaka tufanye nini?

Upendo wa Mungu kwetu sisi ni mkubwa hivi kwamba ametutengenezea njia ambayo kwayo tuweze kusamehewa. Hii ni kwa Yesu Kristo. Imani yetu katika Yesu kama Mwokozi wetu hutupa haki ya kusimama mbele za Mungu. Sisi, ni lazima tukubali kuwa ni wenye dhambi. Wala kabla ya hivyo, Mungu hawezi kufanya kazi mioyoni mwetu.

# ADHABU

MAANDIKO: Warumi 6:1-23

KIFUNGU KIKUU: Warumi 6:23. "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."

## MSHAHARA WA DHAMBI:

Mishahara yetu huja au hutoka kwa watu wale tuwatumikiao au kuwafanyia kazi. Ikiwa hatutaweza kujitoa wenyewe kabisa kwa Mungu katika Kristo, basi Shetani ni Bwana wetu. Mshahara wa huyu Shetani ni mauti. Hatuwezi kuwatumikia mabwana wawili.

## MAUTI:

Hii inazungumzia juu ya kifo cha kiroho. Mshahara wa pekee ambao Shetani aweza kutupatia ni adhabu ya milele katika Jehanam, yaani kutengwa na Mungu. Hana kitu kingine zaidi cha kutoa. Yeye hutunyang anya furaha yetu pamoja na uzima wa milele.

## KARAMA YA MUNGU:

Mungu ana karama (zawadi) ya bure kwa ajili yetu. Hatuhitaji kufanya kazi ili kupata karama hii. Zawadi ni kitu ambacho mtu hukupa. Mungu hutupa sisi zawadi au karama ya uzima wa milele. Ni wajibu wetu kukubali au kukataa karama hii.

## UZIMA WA MILELE:

Hii ndiyo karama ya Mungu. Hii ni zawadi ya kule kuamini

kwetu katika Kristo na kumfuata yeye. Hii inaweza kutupatia furaha tu. Hii ni karama ya milele. Karama hii ni kuwa pamoja na Mungu milele huko Mbinguni.

KATIKA KRISTO YESU:

Karama ya Mungu haipatikani kwa kazi zetu tuzifanyazo. Kilitolewa wakati Kristo alipokufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Mungu alimtoa Mwanawe wa pekee kwa ajili ya dhambi zetu. Yesu naye akatoa maisha yake kwa ajili yetu. Tukipokea karama ya Mungu, Yesu Kristo, kama Mwokozi wetu basi tunao uzima wa milele.

MASWALI:

1. Je! Tunaweza kuwa na mabwana wangapi?

2. Je! Ni mshahara gani ambao Shetani hutupa?

3. Karama ya Mungu kwetu ni nini?

4. Tunawezaje kupata Uzima wa Milele?

Ni lazima uchague Bwana wako. Chagua leo kama ni nani utakayemtumikia. Tumikia Mungu nawe utapata amani. Kubali karama yake, ya uzima wa milele katika Yesu Kristo nawe ufurahie kuishi milele mbinguni.

## UPENDO WA MUNGU

MAANDIKO: Yohana 3:1-21

KIFUNGU KIKUU: Yohana 3:16. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."

JINSI HII MUNGU ALIUPENDA:

Muumba wetu ana mapenzi makuu kuliko wote. Alitupenda sisi hata tulipokuwa tungali wenye dhambi. Upendo wa Mungu hauwezi kupimwa. Upendo wa Mungu hauna mwisho.

ULIMWENGU:

Kiwango kikuu cha upendo wa Mungu kinaonyeshwa katika mapana ya upendo wake. Mungu apenda watu wote ulimwenguni.

HATA AKAMTOA MWANAWE PEKEE:

Hiki ndicho kitendo kikubwa cha upendo. Yesu Kristo ndiye karama kuu. Mungu hakumzuilia mtoto wake. Alitupa sisi zawadi hii kama njia ya kuweza kukimbia toka kwa mauti ya milele, katika Jehanam.

ILI KILA MTU:

Huu ni mwaliko mkubwa ambao umewahi kutolewa. "Ili kila mtu amwaminiye," haina maana ya mtu wa rangi fulani, utajiri, elimu wala mtu toka katika nchi fulani. Mwaliko huu unamwalika

mtu ye yote kuamini katika mpango wake wa wokovu.

AMWAMINIYE:

Mtu mkubwa alikufa kwa ajili ya dhambi zetu. Yesu, mtoto wa pekee wa Mungu, alikufa msalabani kwa ajili yetu. Yeye hakufanya dhambi, bali alichukua dhambi zetu juu ya msalaba ili sisi tuwe huru.

ASIPOTEE:

Ukombozi ule mkuu ambao umewahi kutolewa ni wetu sisi. Kwa kumwamini Yesu sisi tunakombolewa kutokana na kupotea kwetu katika Jehanam.

BALI AWE NA UZIMA WA MILELE:

Hii ndiyo tofauti kubwa. Uhakika mkuu wa karama yake ni hii ahadi yake. Dakika ile tunapomwamini Yesu tunafanywa watoto wa Mungu na tunapewa uzima wa milele. Ahadi yake ni ya wakati huu na wakati wote hata milele. Milele haina mwisho.

MASWALI:

1. Ni nani ana upendo mkuu kuliko wote?

2. Je! Mungu alionyeshaje upendo wake?

3. Je! Anawaalika kina nani kumwamini?

4. Tutafanya nini tupate uzima wa milele?

5. Je! Uzima wa milele ni wa muda gani?

Mungu hakumtuma Mwanawe kuja azihukumu dhambi zetu. Yesu alikuja ili tupate kusamehewa dhambi zetu. Ili tupate msamaha huu ni lazima tuamini kuwa Yesu ndiye Mwokozi. Wokovu wetu unakamilika katika Yesu. Hatuwezi kujiokoa wenyewe.

# KUKIRI

MAANDIKO: Warumi 10:1-11

VIFUNGU VIKUU: Warumi 10:9-10. "Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako yakuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."

## KUAMINI:

Ilikuokolewa, mtu ni lazima aamini moyoni mwake ya kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Ni lazima tuamini ya kwamba Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Na kwamba alizikwa. Pia ni lazima tuamini kuwa Mungu alimfufua toka kwa wafu. Ni lazima tuamini ya kuwa Yesu yungali hai hata leo. Si lazima tuseme maneno tu, ni lazima tuamini katika mioyo yetu.

Watu wengine huamini ya kwamba, kuwa mshiriki wa kanisa huwafanya waokolewe. Lakini kujiunga na kanisa hakuwezi kutuokoa. Ni lazima tumwamini Yesu Kristo kama Mwokozi wetu.

## KUKIRI:

Ni lazima tukiri kwa midomo yetu kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Ikiwa tunaamini kwa kweli kwamba wokovu huja kwa kumwamini Yesu, ni lazima tukiri hivi mbele za wengine. Hatufundishwi juu ya wanafunzi wa siri katika Agano Jipya.

Ni lazima tuone dhambi zetu katika maisha yetu. Ni lazima tusikitishwe na dhambi zetu. Ni lazima tuungame dhambi zetu kwa Mungu. Ni lazima tuombe msamaha. Tuziungamapo dhambi zetu ni lazima tuziache, tusizifanye tena. Ni lazima tumwombe Mungu atusaidie. Ni lazima tukae mbali na majaribu.

WOKOVU:

Hatuokolewi kwa nguvu au kazi zetu. Ni kwa kuamini kile ambacho Mungu ametufanyia. Wokovu ni wetu tunapomwamini na kumkiri Yesu Kristo kama Mwokozi wetu.

MASWALI:

1. Ni lazima tuamini nini ili tuokolewe?

2. Je! Ni lazima tukiri nini?

3. Ni lazima tufanye nini juu ya dhambi zetu?

4. Je! Ni nguvu za nani zituokoazo?

Mungu anatutaka tuokolewe. Anatoa msamaha kwa dhambi zetu. Msamaha huu unakuja kwa njia ya kumwamini Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu. Tusione aibu kuwaambia wengine. Tuwaambie wengine juu ya kipawa kikuu cha Mungu cha wokovu.

## HAKIKISHO

MAANDIKO: 1 Yohana 5:1-13

VIFUNGU VIKUU: 1 Yohana 5:11-12. "Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye huyo Mwana anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."

### USHUHUDA:

Ye yote aaminiye ya kwamba Yesu ni Kristo, amezaliwa na Mungu. Na ye yote aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Mtu aaminiye kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, atakuwa na uhakika wa jambo hili katika maisha yake. Katika Yesu, maisha yako yanatakiwa yawe ushuhuda wa yale Mungu aliyokufanyia. Ikiwa maisha yetu yanamwonyesha Yesu, basi hili ni hakikisho kwamba tumepata kuzaliwa upya.

### UZIMA WA MILELE:

Tunao ushuhuda kwamba Mungu ametupatia uzima wa milele kwa kupitia kwa Mwanawe, Yesu. Yesu alikufa juu ya msalaba kwa ajili ya dhambi zetu. Alizikwa, na Mungu akamfufua toka kwa wafu. Kila amwaminiye Yesu kama Mwokozi, ana uzima wa milele.

### UZIMA UMO KATIKA MWANAWE:

Kwa sababu Yesu alishinda mauti na kufufuka toka kwa kaburi, sisi pia tuna uzima katika yeye. Tunapomwamini Yesu tunashiriki katika uzima wa milele kama watoto wa Mungu. Kumkataa Yesu ni kubaki katika dhambi na kupata mauti ya milele katika Jehanam.

Kutengwa na Mungu ni kifo.

MASWALI:

1. Tunawezaje kujua kama tuna uzima wa milele katika Yesu?

2. Tunawezaje kupata uzima wa milele?

3. Je! Maisha yetu yanapaswa yashuhudie nini?

Mtoto wa Mungu ataonyesha maisha yake kuwa yako kwa Mungu. Imehakikishwa ya kwamba mtu amwaminiye Yesu atapenda awe shahidi kwa wengine. Ukimwamini Yesu kama Mwokozi wako na kwamba yeye ni Mwana wa Mungu, unaweza kuhakikishiwa juu ya wokovu. Maisha yako yanatakiwa yawe ushuhuda ya kwamba Mungu yumo ndani yako. Hakikisho la ushuhuda huu ni imani yako katika Yesu, kuwapenda wengine, kutii amri za Mungu, kuishi maisha ya ushindi pamoja na kuwa shahidi. Usilitilie mashaka neno la Mungu. Usiishi maisha ambayo yatawafanya wengine kushuku uhakika wako.

# USHINDI

<u>MAANDIKO</u>: 1 Wakorintho 10:1-14

<u>KIFUNGU KIKUU</u>: 1 Wakorintho 10:1-14. "Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili."

## <u>JARIBU HALIKUWAPATA NINYI</u>:

Hatuko huru mbali na kujaribiwa na Shetani. Shetani hujaribu kutuweka mbali toka kwa Mungu. Tusiwe watu tusioelewa majaribu ya Shetani, bali heri tujihadhari nayo. Majaribu yamemjia mwanadamu mara kwa mara. Wana wa Israeli walijaribiwa. Majaribu kama hayo yamekuwa ni ya kawaida kwetu siku hizi (hata leo). Shetani ataka kuturarua sisi. Mungu nidye nguvu tunayoihitaji kutukinga kutokana na kujaribiwa na Shetani.

## <u>KAWAIDA YA WANADAMU</u>:

Tamaa mbaya, ibada ya sanamu, uasherati na kutokuwa na furaha kwa Mungu, ni baadhi tu ya majaribu ya kawaida. Yesu alipokuwa nyikani na alipoanza kuona njaa alijaribiwa na Shetani. Yesu alijaribiwa kugeuka toka kwa mapenzi ya Mungu katika maisha yake. Majaribu ambayo ni ya kawaida kwetu yamewahi kuwakuta watu wengine pia. Kwa uwezo wa Mungu waliyakataa majaribu haya. Sisi pia tunaweza kupata ushindi juu ya majaribu kwa uwezo wa Mungu.

MUNGU NI MWAMINIFU:

Mungu huzungumza na mioyo yetu. Huyaongoza maisha yetu kukimbia ibada za sanamu na dhambi ambazo zingetuharibu. Mungu ni mwaminifu kwa kutupa Mwanawe Yesu Kristo aliye kielelezo na Mwokozi wetu. Mungu ni mwaminifu kutupa nguvu ili tuweze kukataa majaribu. Mungu apenda maisha yetu kuwa ya ushindi na yaliyo huru kutorudia tena dhambi.

MLANGO WA KUTOKEA:

Maisha ya ushindi yanapatikana katika Yesu Kristo. Watu wengi hushindwa na majaribu. Maisha na ushuhuda wao huharibika. Wanajitenganisha wao wenyewe na Mungu. Hii imeandikwa kama onyo kwetu. Mungu alimtoa Mwanawe awe mlango wa kutokea toka kwa mauti ya milele, katika Jehanam. Mtu amwaminiye Yesu kama Mwokozi ni mshindi. Ushindi huu, ulio katika Yesu, hutulinda na majaribu. Yesu atatusaidia wakati tunapojaribiwa.

MASWALI:

1. Ni nani atujaribuye ili tufanye makosa?

2. Ni nani atusaidiaye tunapojaribiwa?

3. Je! Tunajaribiwa katika njia zipi?

Tuwe wenye nguvu katika maisha yetu ya Kikristo. Mungu hapendezwi tunaposhindwa na majaribu. Shetani ni lazima akemewe katika Jina la Yesu ili akimbie. Usianguke katika mtego wa Shetani wa majaribu. Mwite Mungu akuokoe. Amini katika mlango wa kutokea, Yesu Kristo. Mungu atakusaidia katika majaribu kama ukimtegemea yeye.

Somo la Saba (7)

# WOKOVU NI WA MUNGU

MAANDIKO: Warumi 8:24-39

KIFUNGU KIKUU: Warumi 8:30. "Na wale aliowachagua tangu asili, hao akawaita; na wale aliowaita, hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza."

## ALIOWACHAGUA TANGU ASILI:

Ni mapenzi ya Mungu kwamba kila mtu aokolewa toka dhambini. Kwa kuwa tuliumbwa kwa mfano wa Mungu, Mungu alitupa hiari ya kuchagua. Mtu kwa hiari yake mwenyewe alichagua kutomtii Mungu. Hii ilimtenganisha mtu na Mungu. Ili kumkomboa mwanadamu Mungu alipanga kutoka asili juu ya wokovu. Aliweka mpango wa wokovu. Ujuzi huu ulijulikana kupitia kwa siku za Agano la Kale. Ujuzi huu ulitimizwa wakati wa kuja kwa Yesu. Roho Mtakatifu huzungumza na mioyo yetu. Kwa sababu hiyo, tunapata tumaini la wokovu. Kile ambacho Mungu alikijua toka zamani tunakigundua wakati tumpokeapo Mwokozi, kwa kumwamini Yesu Kristo. Ili mtu aokolewe, ni lazima anyenyekee chini ya mapenzi ya Mungu.

## AKAWAITA:

Ni lazima tumruhusu Mungu kuchunguza mioyo yetu. Hii itamwezesha Mungu kusema nasi. Tunapomsikiza Mungu tunaweza kujua mapenzi yake kwetu. Tujitoapo kufuata mwito wake tunafanywa watoto wake. Roho Mtakatifu ni mwaminifu katika kutufunulia mwito huu wa Mungu. Mungu anatuita tumjie yeye mwenyewe. Kwa kumwamini Yesu, tunapata njia ya kumfikia Mungu. Kumkataa Mungu ni kinyume cha mapenzi ya Mungu na tunabaki tumepotea katika dhambi.

AKAWAHESABIA HAKI:

Kwa kuitikia mwito wa kumwamini Yesu tunahesabiwa haki ya kuwa watoto wa Mungu. Imani yetu katika Yesu na toba letu la dhambi hutuwezesha kusimama mbele za Mungu. Hatustahili jambo hili ila upendo wa Mungu wa kusamahe hulifanya liwezekane. Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kwamba sisi tuweze kuhesabiwa haki. Mungu alimtoa Mwanawe kuja kutukomboa.

AKAWATUKUZA:

Kama watoto wa Mungu, hakuna kitu kiwezacho kututenganisha naye. Kutukuzwa ni lengo la kila mtoto wa Mungu. Huu ndio wokovu wa mwisho na ulio mkamilifu ambao utatambulikana mbinguni. Mkristo ni mrithi wa haki ya kuzaliwa. Kila mtu atafurahi mbinguni kwa hali timilifu kufuatana na kipimo chake. Kipimo hiki kitafuata kukua kwa mtu na utumishi wake kwa Kristo alipokuwa duniani.

MASWALI:

1. Je! Tuko huru kuchagua, kuukataa au kuukubali wokovu?

2. Mungu anapenda tuchague nini?

3. Je! Mtoto wa Mungu aweza kutenganishwa na upendo wa Mungu.

Wokovu ni wa Mungu. Tunapokea wokovu kwa imani katika mpango wa Mungu. Mpango wake ni kwa Mwanawe Yesu. Yesu alikufa juu ya msalaba na kufufuka toka kaburini. Imani na uaminifu wetu katika Yesu hufanya iwezekane kwa sisi kuwa watoto wa Mungu. Yesu yuko mkono wa kuume wa Baba akituombea.

Somo la Nane (8)

# NEEMA YA MUNGU

<u>MAANDIKO</u>: Wagalatia 3:1-29

<u>KIFUNGU KIKUU</u>: Wagalatia 3:13. "Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti."

<u>ALITUKOMBOA</u>:

Mara kwa mara mwanadamu hujaribu kuweka mpango wake wa wokovu. Hii haiwezekani. Mara kwa mara mtu hujishughulisha kupata wokovu kwa uzuri wake. Kwa asili mtu ni mwenye dhambi. Mara nyingi mtu hujidhania mwenyewe kuwa aliyepokelewa kwa Mungu kwa kuwa mtiifu kwa sheria ambazo zimefanywa na mwanadamu. Njia hii ipo machoni pa mtu wala si ya Mungu. Dhambi zetu zatuhukumu. Mungu tu ndiye awezaye kutuokoa na hukumu hii. Tunapata ukombozi kwa njia ya imani.

Upendo wa Mungu ni mkubwa kwamba alilipa deni la dhambi zetu. Alifanya hivi kwa njia ya maisha ya Mwanawe Yesu. Neema ya Mungu ilitukomboa na kulipa deni ili tupate wokovu.

<u>LAANA</u>:

Dhambi iliweka kila mmoja wetu chini ya laana. Tulitengwa mbali na Mungu. Laana hii iliondolewa na Yesu. Kristo hakufanya dhambi. Alichukua dhambi zetu juu yake na kufa Msalabani. Alikufa, kwamba dhambi zetu ziweze kusamehewa. Alikufa mahali petu ili laana iliyo juu yetu ipate kuondolewa. Katika dakika ya kifo chake msalabani, Mungu alimwacha. Kristo aliteseka na hatimaye

**kushinda laana ya dhambi iletayo mauti ya milele. Kristo alifufuka toka kaburini na kuwa mshindi wa kwanza katika mpango wa Mungu wa wokovu.**

MASWALI:

1. Kwa nini Yesu alikufa msalabani?

2. Ni nini kiliweka laana juu yetu?

3. Je! Laana hii huondolewaje?

Kristo alisulibiwa msalabani ilikutoa wokovu kwetu. Laana ya dhambi iko juu ya kila mtu ambaye hajaamini katika mpango huu wa wokovu. Neema ya Mungu ili tufanyia mpango wa wokovu. Upendo wake kwetu ulikuwa mkubwa kwamba alitoa wokovu ilikuondoa laana ya dhambi. Tunakombolewa kwa kumwamini Yesu kama Mwokozi na kumwomba Mungu atusamehe dhambi zetu. Laana imeondolewa. Tumesamehewa. Tuko huru tokana na kuzuiliwa na Shetani.

## KRISTO NA MUNGU

MAANDIKO: Yohana 10:7-30

KIFUNGU KIKUU: Yohana 10:30. "Mimi na Baba tu umoja."

MIMI NA BABA:

Yesu alikuja ili Mungu, kwa kupitia kwa Yesu, aweze kujionyesha. Kumjua Yesu ni kumjua Baba. Kumwamini Yesu ni kumwamini Mungu. Kukubaliwa katika Yesu ni kukubaliwa katika jamii ya Mungu, hali Mungu mwenyewe akiwa Baba. Kufunuliwa kwa Mungu kama Baba kuliko wazi zaidi, kulikuja kwa njia ya Yesu. Tunaweza kufanyika watoto wa Mungu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo. Kifo chake msalabani kilitoa ukombozi wa wanadamu toka dhambini.

Yesu alijitaja mwenyewe kama mlango. Pia alijitaja kuwa njia ya kuingia mbinguni kwa Mungu. Yesu alisema, "Mimi ndimi njia . . . . Mtu haji kwa Baba ila kwa mimi." Tunaingia katika njia hii kwa imani.

UMOJA:

Mungu na Kristo ni wa moja katika kusudi na mpango wa wokovu wa mwanadamu. Tukiwa na Yesu kama Mwokozi, tunahakikishiwa juu ya uzima wa milele pamoja na Mungu. Njia ya Mungu ya wokovu katika Kristo ni salama. Mtu hawezi kumchukulia Yesu kama Mwokozi bila kwanza kumfikiria Mungu kama Baba wa mbinguni. Kristo hutupatia uzima wa milele. Tunaitwa kondoo katika Biblia. Yesu alijitaja mwenyewe kama Mchungaji Mwema. Tukiwa wake twaifahamu sauti yake na twapenda kumfuata. Huwa pia ni wa Mungu. Ni Baba wa kweli wa wale wanaofanyika watoto wa Mungu tu, kwa imani katika Mwanawe.

MASWALI:

1. Ni nani mlango wa uzima wa milele huko mbinguni?

2. Mtu huingiaje katika mlango huu kufikia uzima wa milele?

3. Je! Kristo hutupa uzima wa namna gani tumpokeapo?

Unaweza kuuliza, "Inawezekanaje kwa mtu kuwa mmoja, tena awe zaidi ya mmoja?" Mungu aliona haja ya mtu kukombolewa kutoka kwa dhambi. Alikuja duniani kwa njia ya Yesu Kristo. Kwa njia hii, Mungu angeweza kutoa wokovu ambao mwanadamu angeweza kuushuhudia.

Mtu ni mtu mmoja. Lakini kwa baba yake yeye ni mtoto, na kwa mke wake yeye ni mume, na kwa watoto wake yeye ni baba! Yeye ni mtu mmoja, ila anageuka kuwa mtu tofauti kwa baba yake, na kwa bibi yake na kwa watoto wake. Mungu na Kristo ni wa moja katika mpango wao wa wokovu. Mpango huu wa wokovu ni kwa watu wote.

# KUSAMEHEWA

MAANDIKO: Luka 15:11-32

VIFUNGUU VIKUU: Luka 15:21, 22, 24. "Yule mwana akamwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena. Lakini Baba aliwaambia watumwa wake, Lileteni upesi vazi lililo bora mkamvike; . . . kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea naye ameonekana. Wakaanza kushangilia."

## NIMEKOSA:

Mtoto alikuwa ameiacha nafasi ambayo ametayarishiwa na babake. Mtoto alitaka kuishi maisha yake mwenyewe. Alikwenda mbali toka kwa baba na kuishi maisha ya dhambi. Maisha haya yalikuwa mabaya. Maisha haya yalikuwa nje ya mapenzi ya baba. Haya yalikuwa ni maisha yaliyotengwa toka kwa baba.

## SISTAHILI TENA:

Biblia inatutaja sisi kuwa kondoo waliopotea. Biblia hutwambia kuwa wote wamefanya dhambi na kutindikiwa na kile Baba yetu wa mbinguni akusudiacho tuwe. Mungu anatupenda. Biblia inatwambia kuwa hata tulipokuwa tungali wenye dhambi Mungu alitupenda bado. Hapendezwi na dhambi zetu. Ungamo letu la dhambi na msamaha wake hufanya iwezekane kwa sisi kusimama mbele zake. Mungu hutukaribisha tunapomwendea.

## VAZI LILILO BORA:

Katika kitabu cha Isaya tunaambiwa kuwa haki yetu yote imekuwa kama matambara yaliyotiwa unajisi. Hatuwezi kuwa na haki kati yetu wenyewe. Mungu ndiye anayeyabadilisha maisha yetu. Tunapotubu na kuomba msamaha, matambara yetu ya dhambi huondolewa.

Na Mungu hutuvisha haki.

MWANANGU ALIKUWA AMEKUFA, NAYE AMEFUFUKA:

Mtoto alipokuwa mbali na babake, hakuwa na uhusiano. Hawakuzungumza. Hawakutembea pamoja. Mtoto alikuwa nje ya ushirika na babake. Baba hakuweza kushirika maisha ya mtoto wake. Baba aliendelea kungojea mtoto wake huku akiwa hajui hali ya mtoto mwenyewe. Mtoto alipomrudia babake, maisha yaliweza kushirikiana tena. Waliweza kutembea na kuzungumza pamoja.

Yesu alisema, "Mimi ndimi njia, na kweli, na UZIMA." Ni kwa kumjia Baba tu, kwa njia ya imani katika Yesu, tunapoweza kupewa uzima. Ni mbele za Mungu tu, tunapoweza kusamehewa.

ALIKUWA AMEPOTEA NAYE AMEONEKANA:

Hapo mwanzoni, mtoto alikataa kile ambacho baba alitoa. Mtoto akaenda zake. Maisha yake yalimpeleka hata nchi nyingine. Aliporudi nyumbani, baba alijua juu ya kurudi kwake. Baba alimngojea mtoto kutafuta njia ya kuweza kurudi nyumbani. Jinsi tuzidivyo kuwa mbali na mpango wa Mungu wa wokovu, ndivyo tubakivyo tukiwa tumepotea katika dhambi zetu. Ni lazima tumjie Baba ili tupate msamaha.

MASWALI:

1. Je! Ni nini hututenganisha na Mungu?

2. Ni kitu gani muhimu ili kupata msamaha wa dhambi?

3. Twawezaje kuja kwa Baba na kupata msamaha?

Hatuwezi kuishi kwa vitu vya kidunia na kuwa na ushirika na Baba yetu aliye mbinguni. Mtoto alitubu dhambi zake. Alitoka mahali pa dhambi alipokuwa. Akaja kwa babake. Mtoto aliomba msamaha wa dhambi zake. Baba alimsamehe. Tunapata msamaha tunapoutafuta toka kwa Baba yetu aliye mbinguni.

# UKRISTO

MAANDIKO: 1 Wakorintho 3:1-23

VIFUNGUU VIKUU: 1 Wakorintho 3:9-11. ". . . ni jengo la Mungu. Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake. Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo."

## NI JENGO LA MUNGU:

Kuna dini nyingi. Lakini kuna Ukristo mmoja tu wa kweli. Ukristo ni kumkubali Kristo kama njia ya Mungu ya wokovu. Mtu huwa Mkristo kwa kumkubali Kristo kama Mwokozi. Ili kuwa kama-Kristo, ni lazima mtu amruhusu Kristo kuwa Bwana wa maisha yake. Unafanyika kuwa makao ya Kristo wakati umpokeapo yeye kama Mwokozi. Unafanywa kuwa jengo la Mungu. Wewe si mali yako mwenyewe. Ili kuwa makao ya Mungu yenye nguvu, huwezi kujenga maisha yako na ugomvi, wivu na mafarakano. Mungu hataishi katika maisha yaliyojaa kiburi na kujipenda mwenyewe. Mungu anatupenda tuishi maisha yanayofuatana na maisha ya Kristo. Maisha yako ya kiroho ni lazima yajengwe kwa uongozi wa Mungu.

## NALIWEKA MSINGI:

Watu walitaka kumtazama Paulo na Apolo kuwa miungu wao. Paulo akawaonyesha ya kwamba yeye na Apolo ni watumishi tu wa Mungu. Mungu aliwatumia hao kuwaonyesha wokovu katika Kristo.

Walikuwa wanaweka msingi, lakini Mungu angejenga juu ya msingi huo. Mkristo ni sehemu ya jengo la Mungu. Paulo aliuliza, "Hamjui ya kuwa ninyi ni hekalu la Mungu na kwamba Roho wa Mungu anaishi ndani yenu?" Mkiruhusu mambo ya mwili kuwatawala ninyi, basi hamruhusu Mungu kuishi na kujenga ndani ya maisha yenu.

MSINGI MWINGINE HAKUNA MTU AWEZAYE KUUWEKA:

Yesu Kristo ndiye msingi tunaohitaji kujenga maisha yetu juu yake. Msingi mwingine wo wote utakuwa mdhaifu na hata kuanguka. Misingi mingine haitalizuia jengo. Ukristo ni wa Kristo wala si wa mtu. Mungu alitoa msingi. Msingi huu uliwekwa katika kifo, mazishi na kufufuka kwa Yesu. Ye yote awekaye imani katika msingi huu ana busara. Cho chote tufanyacho ni lazima kifanywe kwa ajili ya Mungu.

MASWALI:

1. Ni nani angekuwa msingi katika maisha yetu?

2. Je! Ukristo ni nini?

Jenga maisha yako juu ya Yesu. Usiwe mdhaifu. Hatuwezi kuwa na nguvu kwa hekima zetu wenyewe. Hatuwezi kuwa na nguvu kwa kuishi katika dhambi. Hatuwezi kuwa na nguvu kwa kujenga juu yetu wenyewe. Sisi ni makao ya kuishi ya Mungu duniani. Basi iweni wenye nguvu katika yeye.

o

## ASILI MPYA

**MAANDIKO:** Waefeso 4:17-6:9

**VIFUNGU VIKUU:** Waefeso 4:22-24. "Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; mkavae utu upya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli."

### MVUE KWA HABARI YA UTU WA ZAMANI:

Kama Wakristo, tunahitajika tuwe tofauti na watu wasikuwa Wakristo. Tumetoa maisha yetu kwa bwana mpya. Dhambi si njia ya maisha yetu tena. Maisha ya zamani ni njia ya kutembea katika giza la dhambi. Yesu ndiye nuru yetu. Mtu wa zamani hujifikiria nafsi yake tu. Mtu wa zamani amejaa ulafi na uchafu katika nia na moyo wake. Na tuvue hasira, masengenyo, chuki pamoja na mazungumzo mabaya. Biblia hutuambia kuwa tusimpatie nafasi Ibilisi katika maisha yetu. Mtu mpya ni amwonyeshe Kristo katika usemi wake, maisha pamoja na matendo yake.

### MFANYWE WAPYA KATIKA ROHO YA NIA ZENU:

Paulo katika Wafilipi 2:5 alisema, "Iweni na nia hiyo hiyo ambayo ilikuwako pia katika Kristo Yesu." Tunatakiwa tumwigize Yesu katika maisha yetu. Kwa kumchukua Yesu kama Mwokozi, tunajitoa mwenyewe kwa njia mpya ya maisha. Kuna toba ya dhambi. Hii ni kukubali dhambi zetu na kumwomba Mungu atusamehe. Kuna kugeuzwa toka kwa maisha ya zamani mpaka kwa maisha mapya. Hapo huwa na njia mpya ya mawazo.

MKAVAE UTU UPYA:

Mtu mpya ni mfuasi wa Mungu. Ana asili mpya. Hutembea katika upendo badala ya chuki. Amejazwa na Roho wa Mungu badala ya vinywaji viovu. Ni mtu mwenye kuipenda jamii yake. Mtu mpya ana urithi katika Ufalme wa Kristo na Mungu. Hana nafasi ya mambo mabaya kuishi. Mtu mpya hatazini, kudanganya au kuishi katika uongo.

Mtu mpya hutembea katika nuru ya Mungu. Yesu alikuja ili kuleta maisha mapya. Mtu amwaminiye yeye atapata uzima wa milele. Kumwamini Yesu ni kukubali njia mpya ya maisha.

MASWALI:

1. Ni nani aliyekuja kumletea mwanadamu njia mpya ya maisha?

2. Mtu huwa na asili gani kabla ya kuwa mtu mpya katika Kristo?

3. Mtu mpya katika Kristo ataishi namna gani?

Mtu aishiye maisha mbali na Mungu si mnyenyekevu kwa Mungu. Maisha mapya yanatakiwa yawe maisha ya utiifu. Huduma zetu ziwe kwa Mungu. Tuishi maisha ambayo wengine wataona kwamba tuna asili mpya.

Somo la Kumi na Tatu (13)

# NJIA

MAANDIKO: Yohana 14:1-21

KIFUNGUU KIKUU: Yohana 14:6. "Yesu akawaambia, Mimi ndimi njia na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi."

## MIMI NDIMI NJIA:

Mara kwa mara watu wamejishughulisha na mambo ya siku za mwisho. Je! Kuna maisha baada ya kifo?

Yesu alisema, "Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo."

Mungu anataka kwamba wote wamjie. Mungu alimwumba mwanadamu kwa hali ya hiari. Mwanadamu halazimishwi na Mungu. Mungu alitoa njia ya uzima wa milele katika Yesu Kristo, Mwanawe. Kristo alikuja na kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Mtu achaguaye njia hii hupewa uzima wa milele. Hiki ni kipawa cha Mungu kwa ye yote atubuye dhambi na kumpokea Kristo kama Mwokozi. Yesu alisema kwamba yeye ni njia ya kwenda kwa Baba huko mbinguni. Biblia hutuambia kuwa hakuna njia nyingine iliyotolewa na Mungu iletayo uzima wa milele mbinguni. Yesu ametayarisha mahali kwa wafuasi wake. Yesu ndiye njia ya mpango wa Mungu wa wokovu.

## MTU HAJI KWA BABA ILA KWA MIMI:

Yesu ndiye njia ya kumwendea Baba. Ndiye mpatanishi wetu.

Wakati mmoja Yesu alijitaja kuwa mlango. Kiingilio katika uzima wa milele ni Yesu. Kiingilio kwa uzima wa kweli duniani ni Yesu. Mungu alimtuma Mwanawe kwamba kila aaminiye katika yeye apate uzima huu wa milele. Yesu anamwakilisha Baba yake. Kumkataa Yesu ni kumkataa Mungu Baba. Kumkataa Yesu ni kukataa kutembea katika njia ambayo Mungu apenda tufuate duniani.

MASWALI:

1. Ni nani aliye njia ya uzima wa milele?

2. Yesu aliwatayarishia akina nani makao huko mbinguni?

Njia ya Yesu hutuelekeza mbinguni. Mtu huwa mfuasi wa njia hii kwa kumwamini Yesu kama Mwokozi wake. Njia ya Yesu humwelekeza mtu kumwishia Mungu. Tembea katika njia ya Yesu. Ukifanya hivyo Roho Mtakatifu atakuongoza. Yesu alisema, "Mkinipenda, mtazishika amri zangu."

# TOBA

MAANDIKO: Matendo 2:14-41

KIFUNGU KIKUU: Matendo 2:38. "Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

## TUBUNI:

"Tubuni" ni neno lililotumiwa na Petro kuwaambia watu jinsi ya kukimbia mauti ya milele. Petro alikuwa anazungumza na watu waliombulibisha Yesu. Hawakumpokea kama Mwana wa Mungu. Petro alikuwa anahubiri siku ya Pentekosti. Alihubiri njia ya Yesu. Baada ya kusulibiwa Yesu aliwekwa kaburini. Kaburi halikuweza kumzuia. Kama Mwana wa Mungu, Yesu alifufuka na kurudi kwa Baba yake huko mbinguni.

Wakati Petro alipokuwa akihubiri, watu walipata kutambua kwamba Mungu alimfanya Yesu huyo huyo waliyemsulibisha, kuwa Bwana na Kristo hali wao hawakumpokea. Wakamwuliza Petro, "Tufanye nini?" Petro aliwaambia watubu na kumpokea Yesu kama Mwokozi wao. Kutubu maana yake ni mtu kugeuka toka kwa dhambi zake. Mungu atatusamehe dhambi zetu kama tukizitubu na kugeuka toka kwa dhambi hizo.

## MKABATIZWE KWA JINA LAKE YESU:

Watu waliombwa kwamba watambulikane katika Yesu. Msamaha huja kwa njia ya toba. Maisha mpaya huja kwa njia ya toba. Tukiwa na maisha mapya, basi tunahitaji kuyaonyesha kwa wengine. Ni

kwa sababu ya kile Yesu alichotufanyia juu ya msalaba kwamba msamaha wa dhambi unapatikana. Kumwagika kwa damu ya Kristo juu ya msalaba kulileta ondoleo la dhambi. Damu yake iliyomwagika ilifunika dhambi zetu. Mtu hubatizwa katika jina la Yesu Kristo kuonyesha kuwa ameyafilia maisha ya zamani na kwamba ana uzima mpya katika Yesu Kristo.

MTAPOKEA KIPAWA CHA ROHO MTAKATIFU:

Kabla ya Yesu kusulibiwa, aliwaambia watu kuwa angewapelekea kipawa cha Roho Mtakatifu. Alifanya ahadi nao. Aliwaambia kuwa asingewaacha peke yao na hata bila kufarijiwa. Kwa kumwamini Yesu, mtu hupokea kipawa cha kuwapo kwa Roho Mtakatifu. Kuwako kwa Mungu, katika utu wa Roho Mtakatifu, ni kipawa Mungu atupacho tumwaminipo Yesu. Kwa kuwako kwa Roho Mtakatifu, nguvu ya kushuhudia habari za Yesu hutujia.

MASWALI:

1. Kutubu maana yake ni nini?

2. Kwa nini mtu abatizwe kwa jina la Yesu?

3. Mtu hupokeaje kipawa cha Roho Mtakatifu?

Baada ya kusikia Neno la Mungu, watu walitubu dhambi zao. Waliomba msamaha. Ili kuonyesha kwamba wamekubali maisha haya mapya, watu hawa walibatizwa. Walikuwa waaminifu kwa amri ya Mungu.

# KUJIKABIDHI

__MAANDIKO__: Matendo 8:26-39

__KIFUNGU KIKUU__: Matendo 8:37. "Filipo akasema, Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana. Akajibu, akanena, Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu."

## __UKIAMINI KWA MOYO WAKO WOTE, INAWEZEKANA__:

Ni muhimu kile tuaminicho. Ni muhimu kwa yeye tumwaminiye. Towashi wa Kushi alikuwa akisoma Neno la Mungu. Maandiko aliyosoma yalitoka katika kitabu cha Isaya. Towashi alihitaji msaada wa kuelewa yale aliyokuwa akisoma. Mungu alimtuma Filipo kwenda kumweleza maandiko hayo. Filipo alimhubiri Yesu kwa mtu wa Kushi.

Walipokuwa wakiendelea na safari yao, walifika mahali fulani penye maji. Towashi alimwuliza Filipo, "Ona, hapa kuna maji, ni kitu gani kinizuiacho nisibatizwe?" Ndipo Filipo akasema, "Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana."

Warumi 6:4 twasoma, "Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."

## __NAAMINI KWAMBA YESU KRISTO NDIYE MWANA WA MUNGU__:

Filipo alimwambia towashi kuwa kama angeamini kwa moyo wake wote, yale maandiko yasemayo kuhusu Yesu, angeweza kubatizwa. Towashi alijibu kwa kusema, "Naamini kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu." Aliyakabidhi maisha yake kwa Yesu Kristo. Mtu

ni lazima ayakabidhi maisha yake kwa Yesu akitaka kuwa mfuasi wa Yesu. Towashi alitaka kubatizwa, sawa na maandiko yatuambiavyo kuwa ni lazima tubatizwe.

"Aliamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza . . . (towashi) alikwenda zake akifurahi."

MASWALI:

1. Je! Towashi alikuwa akisoma nini?

2. Mungu alimtuma nani kwenda kumsaidia towashi kuyaelewa maandiko yale aliyokuwa akisoma?

3. Filipo alimwambia towashi afanye nini akitaka kubatizwa?

Mungu alitupa Biblia. Anatutaka sisi tulisome Neno lake. Sisi pia twaweza kwenda zetu tukifurahi kama tutaamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Tutatembea katika upya wa uzima, kama tutayakabidhi maisha yetu kwa Yesu Kristo. Je! Umeyakabidhi maisha yako kwa Yesu Kristo?

Somo la Kumi na Sita (16)

# AMINI

MAANDIKO: Matendo 16:14-36

KIFUNGU KIKUU: Matendo 16:31. "Wakamwambia, mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako."

## MWAMINI BWANA YESU:

Paulo na Sila walifungwa gerezani kwa kuhubiri njia ya wokovu. Ilionekana kwamba hakuna tumaini kwao. Lakini walikuwa wana imani. Walimwamini Mwana wa Mungu. Walimwamini na kumfuata Yesu. Hata katika gereza waliendelea kusali na kuimba nyimbo za kumtukuza Mungu.

Mungu alisikia maombi yao. "Ghafula pakawa na tetemeko kuu la nchi, hata misingi ya gereza ikatikisika, na mara hiyo milango ikafunguka, vifungo vya wote vikalegezwa" (mst. 26). Mlinzi wa gereza alifadhaika kuona kuwa milango yote ya gereza imefunguka. Alifikiria kuwa wafungwa wote wametoroka. Alifuta upanga wake na angejiua.

"Ila Paulo akapaza sauti yake kwa nguvu, akisema, Usijidhuru, kwa maana sisi sote tupo hapa" (mst. 28). Mlinzi alikuja huku akitetemeka kwa hofu na kuanguka mbele ya Paulo na Sila. Akawauliza, "Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?"

## NAWE UTAOKOKA:

Mlinzi hakuwa akiuliza juu ya maisha yake ya kimwili kuokolewa. Hakukuwa na haja ya kuogopa. Wafungwa wote walikuwako. Hawakutoroka. Mlinzi alihusika na maisha yake ya kiroho. Inawezekana kwamba alisikia ushuhuda wa Paulo na Sila. Alijua ni kwa

nini waliwekwa gerezani. Aliona uwezo wa Mungu. Alijua kuwa Paulo na Sila walikuwa tofauti na wafungwa wengine. Mlinzi alitaka uzima huo huo uliokuwa na kina Paulo na Sila. Alitaka kuokolewa toka kwa dhambi zake.

PAMOJA NA NYUMBA YAKO:

Mlinzi alimwamini Yesu kama Mwokozi. Aliwapeleka Paulo na Sila nyumbani kwake. Alitaka kushirikiana na watu wa nyumbani mwake kile alichojifunza. Aliwataka waokolewe. Paulo na Sila walizungumza nao. "Wakamwambia neno la Bwana, yeye na watu wote waliomo nyumbani mwake" (mst. 32).

Kupenda kwake kumshirikisha Yesu, kuliwasaidia wengine kuokolewa. Kila mtu ni lazima amwamini Bwana Yesu kwa ajili yake mwenyewe. Mtu hawezi kumwamini Yesu kwa niabu ya mtu mwingine. Lakini tunaweza kushirikiana nao jinsi ya kuweza kuokolewa.

MASWALI:

1. Je! Paulo na Sila walifanya nini wakiwa gerezani?

2. Je! Paulo na Sila walimwambia mlinzi afanye nini apate kuokolewa?

3. Paulo na Sila walizungumza neno la Mungu kwa nani tena mbali na mlinzi wa gereza?

Mlinzi alipomwamini Yesu alipata uzima mpya. Yeye pamoja na watu wa nyumbani mwake walipata furaha. Walifuata mafundisho ya Yesu. Wote walibatizwa.

Somo la Kumi na Saba (17)

## UNYENYEKEVU

MAANDIKO: 1 Yohana 1:1-10

KIFUNGU KIKUU: 1 Yohana 1:9. "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

### TUKIZIUNGAMA DHAMBI ZETU:

Hakuna mtu aliye mkamilifu. Kila mtu amefanya dhambi. "Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu" (mst. 8). Dhambi iko kinyume cha Mungu.

Mara nyingine hatutaki kuziungama dhambi zetu. Kuungama dhambi zetu ni kukubali hatia yetu. Hatuwezi kupewa msamaha bila kuungama. Mungu atausikia moyo wenye kutubu. Ni lazima tujinyenyekeze kwa Mungu na kutafuta msamaha wa dhambi zetu.

### NI MWAMINIFU NA WA HAKI ATUONDOLEE DHAMBI ZETU:

Mungu anapenda kutusamehe sisi dhambi zetu.. Ni mwaminifu wa kutimiza ahadi yake. "Mungu ni mwaminifu ambaye mliitwa na yeye mwingie katika ushirika wa Mwanawe, Yesu Kristo Bwana wetu." (1 Wakorintho 1:9)

Kila ahadi ya Mungu itatimizwa. Yeye husikiza na huhusika siku zote. Hatatusamehe ikiwa hatutaungama dhambi zetu na kuomba msamaha wake. Hatustahili msamaha ila Mungu anatupenda. Upendo wake mkuu ulitoa msamaha kwa ajili yetu. Kutokana na kifo cha Yesu msalabani tunapewa msamaha.

NA KUTUSAFISHA NA UDHALIMU WOTE:

Hatuwezi kujisafisha wenyewe na udhalimu wetu. Lakini tuzingamapo dhambi zetu Mungu hutusafisha. "Bali tukienenda nuruni kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote" (1 Yoh. 1:7).

MASWALI:

1. Ni kina nani wamefanya dhambi?

2. Ni nani aliye mwaminifu kutusamehe dhambi zetu?

3. Tunawezaje kusafishwa dhambi zetu?

Dhambi zetu ziko juu yetu wenyewe. Mungu ni mnyenyekevu kwa kutusamehe na kutusafisha dhambi zetu. Tukiwa tumesamehewa na kusafishwa tutaishi hali ya unyenyekevu kwa Kristo. Tutashirikiana na Wakristo wengine.